

Familia wapendwa,

Ujumbe ufuatao umetoka kwa msimamizi Mapes:

Shule za wilaya la Perry zinafunga mara moja hadi Aprili 5. Wakati wa mapumziko ya spring inayokuja, tutajadiliana tena ikiwa madarasa yataanza tena Aprili 6.

Hakuna wanafunzi au wafanyikazi ambao wamegunduliwa na COVID-19 (virusi vya Corona) wakati huu. Lakini, Idara ya Afya ya Kaunti ya Marion imeelekeza ya kwamba Shule zote za Kaunti ya Marion kufunga kwa sababu ya tahadhari kubwa. Hii inamaanisha kuwa mazoezi au hafla zote zinazohusiana na shule (riadha, vikao vya SAT, programu za muziki, na kadhalika) zimefutwa. Maombezi ya mapumziko ya spring pia yamefutwa.

Katika siku zijazo, utapokea habari kuhusu programu zetu za chakula cha mchana, kuchukua dawa za wanafunzi, masomo ya nyumbani na kadhalika.

Usalama wa wanafunzi na wafanyikazi ndio muhimu wakati huu. Tutaendelea kuweka habari kupitia viyungo vya Kompyuta( tovuti ya shule,facebook, parent square na kadhalika kama inahitajika. Asante